

Mwaliko na Maelekezo ya Zoom Meeting

Ofisi ya Matumizi ya Lugha inakualika kwenye mkutano wa Zoom uliopangwa kwa ajili ya kesi namba _____
Katika mkutano huu utasaidiwa na mkalimani anayetumia Ukalimani wa Lugha wa Papo Hapo wa Zoom.

Kwa mkalimani wa Kiswahili na pande zinazozungumza Kiswahili:

Tafadhali jiunganishe na Zoom kwa kutumia maelezo ya kuingia yaliyo hapa chini **dakika 30 kabla** kuanza usikilizaji wa kesi yako iliyopangwa ili tuweze kukusaidia kutatua matatizo yoyote ya kiufundi na ya sauti unayoweza kuwa nayo.

Ili kujiunga na usikilizaji wa kesi yako kupitia Zoom kwa kompyuta (PC, Mac, au Linux), simu janja (simu ya mkononi inayotumia Apple iOS, au Android), au kompyuta kibao (Apple iPad, au kompyuta kibao inayoendeshwa na Android), tafadhali bofya kiungo hiki:

Kitambulisho cha Zoom Meeting (nambari/msimbo wa utambulisho): _____

Nenosiri la Zoom Meeting: _____

Maelekezo na mapendekezo ya usikilizaji mzuri wa kesi mahakamani kwa kutumia Ukalimani wa Lugha wa Papo Hapo. **Tafadhali soma maelekezo haya kwa makini sana.**

- HII NI MUHIMU SANA: TAFADHALI JIUNGE NA ZOOM MEETING DAKIKA 30 KABLA YA MUDA ULIOPANGWA KUANZA USIKILIZAJI WA WA KESI YAKO.**
- Kama una wakili, tafadhali mwombe wakili wako akusaidie kupakua na kusakinisha Zoom, kusajili na kuingia kwenye akaunti yako, na kujiunga na mkutano KABLA ya usikilizaji wa kesi yako. Kama HUNA wakili, tafadhali mtafute mtu mwenye ujuzi wa kiufundi ambaye anaweza kukusaidia kufanya mambo haya yote KABLA ya usikilizaji wa kesi yako. Kushindwa kufanya hivyo kunaweza kusababisha kuchelewa kutatuliwa kwa kesi yako.
- Kila mshiriki anapaswa kujiunga kwenye Zoom meeting kutoka kwenye kifaa tofauti** (kompyuta, simu janja, kompyuta kibao, n.k.) ili ukalimani wa lugha uweza kufanya kazi. Ikiwa una wakili, wewe na wakili wako hampaswi **kutumia** kifaa kimoja kwa kuwa ni lazima kila mmoja wenu asikilize kwa lugha tofauti.
- Ikiwa umepanga kuhudhuria mahakamani ana kwa ana, tafadhali beba simu janja na spika za masikioni/kipuli masikioni (chenye maikrofoni) kwenye chumba cha mahakama. Ikiwa wakili wako anapanga kwenda kwenye chumba cha mahakama ana kwa ana, wakili wako pia anapaswa kubeba kifaa chake pamoja na spika za masikioni. Kuvaa spika za masikioni au kipuli cha masikioni kutasaidia kuboresha ubora wa sauti na hukuwezesha kumsikia mkalimani vizuri.
- Unapojiunga na mkutano wa kusikiliza kesi yako kupitia Zoom, LAZIMA uwashe sauti yako. Usipowasha, hakuna mtu atayeweza kukusikia unapongea. Tafuta ujumbe ibukizi unaosema "Jiunge kwa kutumia sauti ya kifaa" au lugha kama hiyo.
- Inashauriwa kwamba ujifunze jinsi ya KUNYAMAZISHA na KUWEZESHA SAUTI yako KABLA ya kuanza kwa usikilizaji wa kesi yako. Lazima uhakikishe maikrofoni yako IMENYAMAZISHWA wakati wa usikilizaji wa kesi yako hadi iwe zamu yako ya kuongea. Ama Hakimu au wakili wako atakufahamisha inapokuwa zamu yako ya kuongea. Wakati hili linapofanyika, utawajibika kuwezesha sauti ya maikrofoni yako.
- Inapokuwa zamu yako kuongea, tafadhali ongea kwa ufasaha na polepole.** Kumbuka kwamba mkalimani anapaswa kurudia kila kitu unachokisema, vilevile kama unavyokisema. Tafadhali **PUMZIKA** baada ya kila sentensi chache ili umruhusu mkalimani atafsiri. Inawezekana kwamba maelezo muhimu yanaweza kupotea ikiwa hutaongea polepole na kupumzika mara kwa mara.
- Mkalimani atajiunga na Zoom meeting dakika 30 kabla ya muda uliopangwa kusikiliza kesi yako ili kukusaidia kutatua matatizo yoyote ya kiufundi na ya sauti unayoweza kuwa nayo. Mkalimani angependa kukusaidia kutatua matatizo ya kiufundi na ya sauti, lakini matatizo mengine yanaweza kuwa magumu kutatuliwa mara moja kabla ya muda wa usikilizaji kesi. Ni wajibu WAKO kujiandaa kadri iwezekanavyo kwa kutatua matatizo yoyote makubwa ya kiufundi KABLA kuanza usikilizaji wa kesi yako.